MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.13. Msimu wa Kilimo 2022/23* *Tathmini ya Januari 21-31, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Februari 1-10, 2023*



**MUHTASARI**


- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka zitasaidia katika ukuaji na maendeleo ya mazao
- Kwa ujumla zao la mahindi katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka yapo katika hali ya kuridhisha.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanahimizwa kuzingatia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Hali hii iliendelea kuusukuma ukanda wa mvua juu kaskazini katika maeneo ya kusini na magharibi mwa nchi. Joto la bahari la juu ya wastani magharibi mwa bahari ya Hindi lilisababisha kutokea kwa migandamizo midogo. Katika tabaka la chini upepo uliendelea kuvuma kutokea magharibi hususan katika nusu ya kwanza ya dekadi, na kusukuma hewa yenye unyevunyevu kutoka kwenye misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi. Hali hii ilikuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha mifumo ya mvua katika baadhi ya maeneo ya magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi, maeneo ya kati mwa nchi, ukanda wa pwani, ukanda wa kusini, na ukanda wa Ziwa Victoria. Pia kuimairika kwa wimbi anga katika bahari ya Hindi (MJO), hususan nusu ya kwanza ya dekadi kulichangia upatikanaji wa mvua katika baadhi ya maeneo ya nchi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2023

Katika nusu ya kwanza ya dikadi hii maeneo mengi ya nchi yalipata mvua. Kiasi cha mvua cha zaidi ya milimita 100 kimerekodiwa katika mkoa wa Ruvuma. Hata hivyo, maeneo mengi ya mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba yamepata kiasi cha mvua cha chini ya milimita 10 kama inavyoonekana katika kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Januari 21-31, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2023

Mvua zilizonyesha katika dikadi hii zimeongeza unyevunyevu katika udongo ambao umesaidia ukuaji wa mazao.
Kwa ujumla mahindi katika maeneo yanayopata mvua za ***Msimu*** yapo katika hali ya kuridhisha.
Katika mkoa wa Kigoma na Tabora mahindi yapo katika hatua ya kubeba.
Kwa maeneo yanayolima mpunga hususan katika mikoa ya Tabora, Mbeya na Rukwa, wakulima wameen-

delea na upandaji.

Kwa upande mwingine katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan Kagera na Simuyu wakulima wameanza shughuli za uvunaji wa mahindi.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori umeendelea kuimarika katika maeneo mengi nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde vimeendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu wakati ile iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuusukuma ukanda mvua kuelekea kaskazini kwa baadhi ya maeneo ya nchi. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi na wastani hadi chini ya wastani kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Katika tabaka la chini upepo unatarajiwa kuendelea kuvuma kutokea magharibi hususan katika nusu ya kwanza ya dekadi, hali hii inatarajiwa kuendelea kusukuma hewa yenye unyevunyevu kutoka kwenye misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi. Hali ambayo kwa kiasi kikubwa itachangia kuimarisha mifumo ya mvua katika baadhi ya maeneo ya magharibi, nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa pwani, kusini, kati na ukanda wa Ziwa Victoria hasusan katika nusu ya kwanza ya dekadi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2023

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2023

Mvua zinazotarajiwa hususan katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo ambao utasaidia ukuaji na maendeleo ya mazao.

Wakulima hususan wanaopata mvua za ***Msimu***, wanashauriwa kuendelea na shughuli za palizi, uwekaji mbolea, kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea kwa kufuata ushauri wa maafisa ugani.

Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, za kwenye maziwa makuu na baharini ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 1-10, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo, jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.



Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)